JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI
JIMBO LA VUNJO

# TAARIFA KWA UMMA

## KUHUSU KUSITISHA UCHAGUZI KATIKA KATA YA KIRUA VUNJO MAGHARIBI

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

Kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 71(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 na kwa barua yenye Kumb. Na CMV/U.30/10/VOLII/45 ya tarehe 21 Oktoba, 2025 kutoka kwa Katibu wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Moshi nimepokea taarifa ya kifo cha Ndugu **John Boniface Kessy** aliyekuwa mgombea wa nafasi ya **Udiwani** Kata ya **Kirua Vunjo Magharibi** kupitia **Chama cha Mapinduzi**.

Kutokana na kutokea kwa kifo hicho, Uchaguzi wa Udiwani katika Kata ya Kirua Vunjo Magharibi Jimbo la Vunjo **UMESITISHWA** kuanzia 21 Oktoba, 2025. Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 71(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi itatoa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali na itapanga tarehe nyingine ya uteuzi wa wagombea ambapo taratibu za uchaguzi wa Udiwani katika Kata husika zitaanza upya.

Hivyo, uteuzi wa wagombea katika kata ya Kirua Vunjo Magharibi na taratibu za uchaguzi zataanza upya.

**"KURA YAKO HAKI YAKO JITOKEZE KUPIGA KURA"**

Imetolewa na:

Lucas Msele
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**
**JIMBO LA VUNJO.**
**21 Oktoba, 2025**

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
JIMBO LA VUNJO
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI

UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025
Kura Yako Haki Yako Jitokeze Kupiga Kura